# ARUSHA MEAT COMPANY LTD.

P.O.BOX 14167

TANZANIA

TEL: +255272970304

Mob: +255734026767

E-mail: arushameatcompany@yahoo.com


AMCL/TND/110/20 11/06/2026

## TANGAZO LA ZABUNI

### 1. UTANGULIZI

Arusha Meat Company Limited (AMCL), ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma za uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali.

### 2. LENGO LA KAZI

Lengo kuu la kazi hii ni kuandaa Sera ya Rasilimali Watu itakayoweka mfumo madhubuti wa usimamizi wa wafanyakazi, kuimarisha utendaji wa kazi, ustawi wa wafanyakazi, uwajibikaji, uwazi na uzingatiaji wa sheria za kazi nchini Tanzania.

### 3. MAJUKUMU YA MSHAURI ELEKEZI

Mshauri Elekezi atatarajiwa kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kufanya tathmini ya mifumo na taratibu zilizopo za usimamizi wa rasilimali watu;

ii. Kufanya mashauriano na menejimenti na wadau muhimu;

iii. Kufanya uchambuzi wa mapungufu yaliyopo katika usimamizi wa rasilimali watu;

iv. Kufanya ulinganisho wa sera na mifumo bora ya usimamizi wa rasilimali watu;

v. Kuandaa rasimu ya Sera ya Rasilimali Watu;
vi. Kuwasilisha rasimu kwa Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya maoni;
vii. Kufanyia kazi maoni yatakayotolewa;
viii. Kuwasilisha nakala ya mwisho ya Sera ya Rasilimali Watu katika mfumo wa soft copy na hard copy.

## 4. SIFA ZA MSHAURI ELEKEZI

**Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:**

i. Uzoefu wa kuandaa Sera za Rasilimali Watu na mifumo ya kiutawala;
ii. Uelewa wa kina wa Sheria za Kazi za Tanzania na kanuni zake;
iii. Angalau miaka mitatu (3) ya uzoefu katika kazi zinazofanana;
iv. Wataalamu wenye taaluma za Usimamizi wa Rasilimali Watu, Sheria, Mahusiano Kazini, Utawala wa Biashara au taaluma zinazohusiana;
v. Uzoefu wa kufanya kazi na taasisi za umma, mashirika au kampuni za uzalishaji utakuwa faida ya ziada.

## 6. NYARAKA ZINAZOTAKIWA KUWASILISHWA

Waombaji wanatakiwa kuwasilisha:

i. Andiko la Kiufundi (Technical Proposal) likionyesha uelewa wa kazi, mbinu za utekelezaji na ratiba ya kazi;
ii. Wasifu wa kampuni (Company Profile);
iii. Wasifu wa wataalamu wakuu (CVs);
iv. Andiko la Gharama (Financial Proposal);
v. Nakala za vyeti vya usajili wa kampuni (CERTIFICATE OF INCORPORATION na TAX IDENTIFICATION NUMBER & BUSINESS LIVENCE);

Mapendekezo ya Kiufundi na Kifedha yawasilishwe katika bahasha zilizofungwa vizuri na kuandikwa "DEVELOPMENT OF HUMAN RESOURCE POLICY"

NB: Waombaji wanatakiwa kufika katika Ofisi ya Idara ya Manunuzi na Ugavi, Arusha Meat Company Ltd-Sakina kuanzia tarehe 11/06/2026 hadi siku ya Tarehe 23/06/2026 siku za kazi, kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni, kwa ajili ya kuchukua nyaraka rasmi za zabuni.

Tarehe ya mwisho ya kukabidhi zabuni ni 23/06/2026, saa 04:00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa rasmi tarehe 23/06/2026, saa 04:01 Asubuhi mbele ya waombaji au wawakilishi wao.

Nyote mnakaribishwa.

……………………………………

**JONAS E. AYO**
**KAIMU MENEJA MKUU**
**ARUSHA MEAT COMPANY LIMITED**

ARUSHA MEAT COMPANY LTD. P.O. Box 14167 ARUSHA - TANZANIA